# MAMBO 10 MUHIMU YANAYOHUSU MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA SHULENI

## MAANDALIZI YA KUFUNGULIWA KWA SHULE KWA AJILI YA WAKUU WA SHULE KATIKA KUPAMBANA NA COVID-19

### 1 UNAWAJI MIKONO NA MAJI TIRIRIKA

Kuwepo kwa vifaa vya kunawia mikono kwa sabuni katika maeneo ya kuingia shuleni (maji yanayotiririka, ndoo zenye bomba au sehemu za kunawa mikono za pamoja) kukiwa na mabomba yenye maji ya kutosha katika umbali unaopendekezwa ili walimu, wanafunzi, wafanyakazi na wageni waweze kunawa mikono kabla ya kuingia shuleni. Vyoo vya shule viwe na vifaa vya kunawia mikono vinavvofanya kazi vikiwa na sabuni na maji. Vifaa vya kunawa mikono vifikiwe na watu wote ikiwemo walemavu.

### 2 UWEPO NA UPATIKANAJI WA MAJI

Kuhakikisha maji yanakuwepo kwa ajili ya kunawa mikono, kunywa na matumizi mengine. Kwa maeneo yenye uhaba wa maji ni vema shule zikaongeza uwezo wa kuhifadhi maji kwa kushirikiana na jamii zilizo karibu na shule au kuwaomba watoto (wanafunzi) kuleta maji toka nyumbani ama kuchota maji kutoka chanzo cha maji kilichoko karibu na shule.

### 3 UWEPO WA VIFAA NA MAHITAJI MUHIMU YA USAFI

Kuhakikisha kunakuwepo na mahitaji yanayotosheleza idadi ya watu. Ni muhimu kuhakikisha kuna kuwepo na sabuni (za vipande au za maji), vitakasa mikono (vyenye alikoholi angalau asilimia 70) na sodium hypochlorite kwa ajili ya kufanya usafi na kuangamiza vijidudu vya maradhi. Kutumia dawa za kuangamiza vijidudu iliyozimuliwa hadi asilimia 0.1, matumizi ya sponji, fagio, ndoo na vifaa kinga kama barakoa na vikinga mikono (glavu) kwa wanaofanya usafi. Dawa za kuangamiza vijidudu vya maradhi vyenye alikoholi asilimia 70 inaweza kutumika katika kufanya usafi.

### 4 USAFI NA KUANGAMIZA VIJIDUDU VYA MARADHI

Kuhakikisha kwamba usafi wa kuangamiza vijidudu vinavyoweza kusababisha maradhi unafanyika kutokana na miongozo ya kitaifa na kimataifa. Maeneo yote yanayoweza kuguswa kwa mikono au sehemu nyingine za mwili yanatakiwa kupewa kipaumbele katika usafi na kuangamiza vijidudu vya maradhi. Daima usafi unatakiwa kufanyika kwa kutumia sabuni katika maeneo ambayo ni rahisi kuguswa na mwili kwa kutumia sabuni za vipande au za sabuni za maji. Kukadiria muda unaohitajika kwa wafanyakazi wanaofanya usafi na kuangamiza vijidudu vya maradhi ili usafi ufanyike vizuri. Nakuhakikisha wafanyakazi wanaofanya usafi wanavaa barakoa na vikinga mikono (glavu). Ni muhimu kuhusisha umoja wa wazazi na walimu, wanajamii na wanafunzi katika masuala ya usafi. Hakikisha kwamba maeneo ya kunawa mikono na vifaa ya chooni vinakuwa safi na katika ubora unaohitajika.

### 5 UHIFADHI WA TAKA

Hakikisha kwamba vifaa ya kuwekea taka vinakuwepo darasani, katika vyoo na katika maeneo yote yanayofikika katika maeneo ya shule ikiwa pamoja na kumwaga taka zilizokusanywa kila siku kufuatana na muongozo au mfumo wa uhifadhi wa taka.

### 6 KUZINGATIA UMBALI

Hakikisha kwamba wanafunzi na walimu wanazingatia kukaa katika umbali unaopendekezwa wa angalau mita moja kutoka mtu mmoja hadi mwingine (kama inavyopendekezwa na miongozo ya kitaifa). Wanafunzi wafike shuleni kwa kubadilishana zamu, kusimamia muda wa kuingia na kutoka shuleni na wakati wa mapumziko, kuweka umbali unaohitajika kati ya dawati na dawati, kufundishia nje ya darasa au kuhakikisha madirisha ya darasa yanakuwa wazi. Kama inawezekana chora mistari inayoonesha umbali ambao wanafunzi wanatakiwa kujipanga au kukusanyika (katika maeneo ya choo au katika sehemu za kunawa mikono).

### 7 KUANZISHA TIMU ZA UFUATILIAJI

Wapangie wafanyakazi wa shule (walimu na wafanyakazi wengine kama wafanya usafi na walinzi, watunza bustani na wanafunzi wenye umri mkubwa, wanajamii na klabu za maji na usafi wa mazingira) kusimamia maeneo ya kunawia mikono na chooni (upatikanaji wa sabuni, maji, ukarabati, kusimamia taratibu/tabia za kunawa mikono na kukaa katika umbali unaopendekezwa.

### 8 MAFUNZO

Kufanya mafunzo kwa walimu na wafanyakazi wote shuleni na wanajamii juu ya masuala ya maji na usafi wa mazingira katika kupambana na COVID-19 ili kuwawezesha kutambua majukumu yao. Kuhakikisha kwamba walimu wanawafundisha wanafunzi, kwa kutumia vitini vya mafunzo, juu ya usafi kwa kuzingatia umri.

### 9 MADODOSO YA TAARIFA

Kuwepo kwa madodoso ya taarifa (yenye tarehe, muda wa kuingia, muda wa kutoka na jina la mfanyakazi wa zamu) kwa walimu na wafanyakazi wengine ili kuhakikisha kwamba majukumu yote yanafanywa kila siku kwa ufanisi unaohitajika. Madodoso haya yanaweza kuwa mahususi kwa:

- Sehemu za kuingia shuleni (tabia/taratibu za kunawa mikono, maeneo ya kunawa mikono, upatikanaji wa sabuni na maji)
- Darasani (shughuli za usafi na kuangamiza vijidudu vya maradhi)
- Vyooni na uhifahi wa taka

### 10 UHAMASISHAJI WA USAFI MASHULENI NA KWENYE JAMII

Kuanzishwa kwa utamaduni/tabia ya kunawa mikono shuleni na kuhamasisha mabadiliko ya tabia ya usafi katika jamii. Kusisitiza wafanyakazi wote (walimu na wasio walimu) wafanye kazi kwa pamoja kujenga utayari wa kushughulikia majanga na kuhakikisha kwamba elimu inasonga mbele na shule zinabaki kuwa sehemu safi na salama ikiambatana na kuwatambua waleta mabadiliko wa masuala maji na usafi wa mazingira katika shule na jamii.

CONTACT: WinS-COVID-19@susana.org

FURTHER INFORMATION: www.susana.org

- '10 IMMEDIATE WinS ACTIONS' (latest version): https://bit.ly/367F7ur
- KNOWLEDGE MAP 'WASH in SCHOOLS & CORONAVIRUS': https://bit.ly/2JDvM39
- 'SAFE BACK TO SCHOOL: A PRACTITIONER'S GUIDE': https://bit.ly/2zS3UHr



german cooperation DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT — giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH — unicef — Save the Children — WaterAid

7th July 2020 // Mtandao wa maji na usafi wa mazingira katika shule unaojulikana kama WinS network (GIZ, UNICEF, Save the Children, Water Aid na mashirika mengine) ni mtandao wa mashirika ya kimataifa unaowaleta pamoja wadau wa maji na usafi wa mazingira kutoka katika taasisi mbalimbali zaidi ya 60 duniani.

cc BY NC ND